



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOSA



KDC/PF.20/1

21 Julai, 2022

**TANGAZO LA KUITWA KWENYE USAILI**


Mwenyekiti wa kamati ya sensa wa wilaya ya Kilosa (Mkuu wa Wilaya), anapenda kuwajulisha waombaji wa ajira za muda za Sensa ya Watu na Makazi kwa nafasi za Karani wa Sensa, Msimamizi wa Maudhui na Msimamizi wa TEHAMA kupitia tangazo la kazi la tarehe 05 Mei 2022 wameitwa kwenye usaili.

Usaili kwa nafasi za Karani wa Sensa na Msimamizi wa Maudhui utafanyika tarehe 22/07/2022 kuanzia saa 2:00 asubuhi katika ofisi ya kata uliyoombea. Kwa nafasi ya Msimamizi wa TEHAMA usaili utafanyika ukumbi wa Halmashauri uliopo makao makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa tarehe 22/02/2022 saa 2:00 asubuhi.

Wasailiwa walioitwa kwenye usaili wanapaswa kuzingatia maelekezo yafuatayo:

1. Kila msailiwa anatakiwa kufika kwenye usaili akiwa na cheti halisi cha kidato cha nne (Original Certificate)
2. Kufika na kitambulisho kwa ajili ya utambuzi kati ya vifuatavyo- Kitambulisho cha Taifa(NIDA), Kitambulisho cha mpiga kura, Leseni ya udereva, Hati ya kusafiria au Kitambulisho cha bima ya afya au kitambulisho chochote kinachotambuliwa kisheria.
3. Waombaji kwa nafasi ya Msimamizi wa TEHAMA wanapaswa kuja na vyeti halisi vya taaluma.
4. Waombaji ambao majina yao hayajaorodheshwa wahesabu kuwa maombi yao hayakukidhi vigezo vya kuitwa kwenye usaili.

Nawatakia utekelezaji mwema.

  
Exavery Luyagaza  
KATIBU WA SENSA WILAYA  
KILOSA

